RISALA YA UTII YA WANANCHI WA WILAYA YA ILALA

KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI KATIKA

MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU

TAREHE 29 MEI, 2017

Mheshimiwa Rais,

Awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwa kutupatia nafasi hii adhimu ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru katika Wilaya ya Ilala. Tunayo furaha kuukaribisha Mwenge wa Uhuru hapa wilayani ili ukimbizwe sehemu mbalimbali kuona, kuzindua na kuhamasisha shughuli za maendeleo zinazotekelezwa kwa ushirikiano wa serikali na wananchi, pamoja na kudumisha **Amani** na **Upendo** ndani na nje ya wilaya yetu.

Mheshimiwa Rais,

Wilaya ya Ilala ina eneo la Kilomita za mraba 210 ambapo asilimia 75 ya eneo hilo ni eneo la mjini. Wilaya hii imepakana na Wilaya za Temeke na Kigamboni kwa upande wa Kusini na Kusini Mashariki, Wilaya za Kinondoni na Ubungo kwa upande wa Kaskazini, Mkoa wa Pwani kwa upande wa Magharibi na bahari ya Hindi katika ukanda wa pwani wenye urefu wa Km. 10 upande wa Mashariki. Wilaya ya Ilala imegawanyika katika Tarafa tatu (3); za Kariakoo yenye Kata 13 na Mitaa 23, Ilala yenye Kata 14 na Mitaa 75 na Ukonga yenye kata 9 na Mitaa 61 na kufanya jumla ya Kata 36 na Mitaa 159.

Mheshimiwa Rais,

Kwa kuzingatia hoja, vipaumbele na Mikakati ya Serikali ya Awamu ya tano, Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2017 umebeba kauli Mbiu isemayo **"*Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi yetu*"**. Pamoja na Kauli Mbiu hii, Mbio za Mwenge wa Uhuru zimeendelea kubeba Ujumbe wa Kudumu wa "***Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, tuwajali na tuwasikilize watoto na vijana*"**; wa pili "***Tuungane kwa pamoja dhidi ya rushwa kwa maendeleo, amani na***

usalama wa Taifa letu"**;** Tatu, "***Tanzania bila ya maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI, inawezekana ifikapo mwaka 2030"*** na mwisho **"*Shiriki kutokomeza malaria kabisa kwa manufaa ya Jamii"***

Kujenga na Kukuza Uchumi wa Viwanda Tanzania

Mheshimiwa Rais,

Ili kuhakikisha mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la taifa unaongezeka na kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imeweka mikakati shirikishi ya uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa Viwanda kama ifuatavyo;

- Kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji EPZ (Export and Processing Zone) katika Bonde la Msimbazi, Msongola na Vingunguti ambao upo chini ya mradi wa PMM. Sambamba na kutenga mitaa ya viwanda vidogo vidogo kama Gerezani na maeneo ya minada; Pugu, Gongolamboto, Kinyerezi na Tabata
- Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo, vya kati na vikubwa kwa njia ya Vyombo vya habari, Semina, Mikutano, mafunzo/kongamano kwa wananchi na wadau pamoja na kujenga mahusiano na Miji rafiki nje ya Tanzania.
- Kuboresha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kama barabara chini ya mradi wa DMDP, barabara za juu za makutano ya TAZARA, Upanuzi wa Kiwanja cha ndege cha Mwalimu Nyerere (JNIA) unaogusa maeneo ya Kipawa, Kipunguni na Kigilagila, Uimarishaji wa Nishati ya Umeme wa uhakika katika Mradi wa Kinyerezi I&II.
- Kuendelea kuimarisha Ulinzi na Usalama katika Halmashauri yetu ili kujenga Imani ya Usalama ya Wawekezaji na Mali zao.

- Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kwa kushirikiana na wananchi imelenga kuboresha masoko yake ya Kisutu, Buguruni, Ilala, Kigogo Fresh, Kerezange, Kinyerezi, Kivule na Tabata Muslim ili kuuzia bidhaa zitakazo zalishwa nchini.

Vita dhidi ya Rushwa

***Mheshimiwa Rais*,**

Kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) tumeendelea kupambana na vitendo vya rushwa kwa kuchunguza, kukamata na kuwapeleka watuhumiwa mahakamani, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 taarifa 255 za rushwa zilipokelewa, majalada 34 ya uchunguzi yamefunguliwa, Mashauri 23 yanaendelea mahakamani, kati ya hayo Sita (6) yakiwa mapya na mawili (2) yamekamilika na watuhumiwa walikutwa na hatia.

Ili kuhakikisha tunatokomeza vitendo vya rushwa kwa kushirikiana na TAKUKURU tunaendelea kutoa elimu ambapo mwaka 2016/2017 tulifanya semina 16, warsha 4, mikutano ya hadhara 15 kwa taasisi za polisi, maji, Afya na huduma za jamii pamoja na kuanzisha klabu 19 za wapinga rushwa katika shule mbalimbali za sekondari.

Mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya

Mheshimiwa Rais,

Tatizo la dawa za kulevya limeshamiri na kuathiri afya na ustawi wa watanzania na hasa vijana. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya waathirika 509 walipata tiba,(wanaume 493 na wanawake 16). Kwa kutambua hilo, Wilaya ya Ilala imeongeza juhudi za kupambana na tatizo hilo kwa kwa kufanya yafuatayo;-

- Kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali juu ya madhara ya matumizi ya dawa hizo. Elimu hii ilitolewa katika za Vingunguti, Kiwalani Kivukoni, Mchikichini, Jangwani, Kipawa, Mnyamani, Minazimirefu, Ilala, Tabata, na Buguruni. Ambapo zaidi ya Dada Poa na Vijana Waathirika wa dawa za kulevya 560 walipata elimu hiyo.
- Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za kulevya kuendeleza msako wa kuwakamata walewote wanaojihusisha na uingizaji, usambazaji, wauzaji na watumiaji na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kutokana na juhudi hizo, jamii imeanza kuelewa madhara yatokanayo na dawa za kulevya na waathirika wanahamasika kupatiwa tiba ya methadone ambayo hutolewa na Serikali.

Mapambano dhidi ya Ukimwi

Mheshimiwa Rais,

Kama zilivyo Manispaa nyingine za Jiji la Dar-es-salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala inafanya kampeni mbalimbali za kudhibiti VVU na UKIMWI kwa kuzingatia sera na miongozo ya kitaifa. Kiwango cha maambukizi ya VVU ni **asilimia 7.1%** ikilinganishwa na kiwango cha Kitaifa cha **asilimia 5.1**% na kimkoa **asilimia 6.9**.

Hivyo, ili kupunguza kiwango hicho na kutekeleza dhamira ya nchi na Jumuiya ya Kimataifa ifikapo mwaka 2030, Halmashauri ya manispaa ya Ilala imedhamiria kufanya yafuatayo;-

- Kuendelea kutoa elimu na huduma ya Upimaji wa VVU kwa hiari na ushauri nasaha. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2016, huduma ya Upimaji wa VVU ilitolewa katika vituo vya afya **167 na** jumla ya watu **281,334** (wanaume 121,753 na wanawake 159,581) walipimwa. Kati yao **13,831** (wanaume 5,027 na wanawake 8,804) sawa na asilimia **4.9%** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU.
- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuendelea kutoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT OPTION B^+). Jumla ya kina mama wajawazito **51,768** walipatiwa huduma ya ushauri nasaha na kupima kwa hiari VVU, kati yao **1,523** sawa na **asilimia 2.9** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU.
- Hadi kufikia Desemba 2016, jumla ya vikundi 40 vya VICOBA vyenye mtaji wa **Tshs 531,525,500** vilianzishwa kwa watu wenye VVU na UKIMWI ili kujiongezea kipato.

Mapambano dhidi ya Malaria

Mheshimiwa Rais,

Ugonjwa wa malaria ni moja kati ya magonjwa kumi yanayoongoza katika vituo vya kutolea huduma. Takwimu zinaonesha mwaka 2016 kati ya wagonjwa wa nje (OPD) 1,740,584 waliotibiwa, asilimia 7 waligundulika na ugonjwa huo ikiwa ni pungufu kwa asilimia 2.8 ya mwaka 2015. Mpango huu wa kupunguza maambukizi ya malaria

unaenda sambamba na lengo la kitaifa la kufikia chini ya asilimia 1% ifikapo 2020. Ili kufikia malengo hayo Halmashauri imedhamiria kufanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha wananchi kushiriki kuangamiza mazalia ya mbu na kupima afya zao pale wanapohisi dalili za malaria sambamba na kuweka mazingira katika hali ya usafi.
- Kuelimisha na kuhamasisha matumizi sahihi ya vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu. Kwa kutekeleza hili, jumla ya vyandarua **725,866** viligawiwa kwenye kaya **480,823** kati ya kay**a 353,788** zilizolengwa mwezi Januari, 2017.

Uwezeshaji wa Vijana Kiuchumi

Mheshimiwa Rais,

Katika kipindi cha Julai - Disemba, 2016, Vyama vya Akiba na Mikopo-SACCOS nane (8) na Vyama mchanganyiko viwili (2) vimesajiliwa na kuelimishwa; Washiriki 505 kutoka Kata 8 za Chanika, Msongola, Kipawa, Vinginguti, Kivule, Kiwalani Majohe na Kitunda zilipata mafunzo. Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile Plan, VSO, Jumuia ya Ulaya, UWIKI, vijana 884, wakiwemo wanaume 421 na wanawake 463 kutoka kata 23 za Tarafa za Ukonga na Ilala wamepata mafunzo ya elimu ya ujasiriamali.

Halmashauri ya manispaa ya Ilala imeendelea kutenga 5% ya fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya vijana ambapo imeingiza kwenye akaunti ya Mfuko wa Mikopo nafuu kwa Wanawake na Vijana kiasi cha Sh. Bilioni 1,250,000 hadi kufikia mwezi Disemba, 2016. Kwa kipindi cha 2015/16 na 2016/17 Kufikia Machi, 2017 jumla ya Sh. 1,579,530,000 zilikuwa zimekopeshwa kwa vikundi 900. Wanawake 3,470 na vijana 1,399.

Mheshimiwa Rais,

Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wilaya ya Ilala imepanga utekelezaji miradi yenye thamani ya Sh Bilioni **98,704,830,810.00** zikiwemo Sh **32,581,200,392.00** fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri, Sh **65,523,630,418.00** fedha za ruzuku kutoka serikali kuu pamoja na Wafadhili na **Sh. 600,000,000.00** mchango wa wananchi. Ambapo, mwenge wa Uhuru katika Wilaya ya Ilala utapitia jumla ya

miradi ya maendeleo 8 ambapo utafanya shughuli ya kuweka mawe ya msingi, utakagua, utazindua na kufungua miradi ambayo yote kwa pamoja ina thamani ya shillingi Bilioni **14,888,864,051**

Mheshimiwa Rais,

Tunapenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe Binafsi, na Serikali yako ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri mnayoendelea kufanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Ilala na Tanzania kwa jumla bila kujali Dini, Rangi, Kabila au Itikadi ya Chama. Tunaomba, "**Mwenyezi Mungu Akubariki"**.

Sisi wakazi wa Wilaya ya Ilala tunazidi kukukaribisha tena na tena katika Wilaya yetu kuja kushuhudia jinsi tunavyonufaika na miradi iliyotembelewa na Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu 2017. Tunamtakia Kiongozi wa mbio za Mwenge pamoja na timu ya wakimbiza Mwenge wa Uhuru-Kitaifa afya na safari njema katika kuhamasisha maendeleo maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.

Mungu Ubariki Mwenge wa Uhuru

Sophia Mjema

MKUU WA WILAYA YA ILALA